**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

---

Ofisi ya Bunge
S.L.P 941
Dodoma

**APRILI, 2018**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

---

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi nyingine ya kukutana hapa Dodoma katika Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Bunge la 11.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6 (2)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu.

Aidha, Kanuni ya 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inatoa Mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia. Jukumu hili la Uchambuzi wa Bajeti linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo nchini, iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2017/2018

kuanzia tarehe 14 hadi 18 Machi 2018. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti za Wizara na Taasisi inazozisimamia kuanzia tarehe 23 hadi 29 Machi, 2018 ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu ina Mafungu 6 ya bajeti kama ifuatavyo;

i) **Fungu 37** - Ofisi ya Waziri Mkuu,
ii) **Fungu 25** - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu,
iii) **Fungu 65** – Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu,
iv) **Fungu 15** - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA),
v) **Fungu 61** - Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), na
vi) **Fungu 27** - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo Manne yafuatayo:-

i) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;
ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;
iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na;
iv) Maoni na Ushauri wa Kamati

## 2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Orodha ya Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

a) **Mradi Na. 6351** – Ujenzi wa Majengo **(Fungu 37)**
b) **Mradi Na. 6575** – Kujiandaa na Kukabili Maafa **(Fungu 37)**
c) **Mradi Na.5306** - Kuimarisha Taarifa za Mabadiliko ya Tabianchi na Mifumo ya Tahadhari **(Fungu 37)**
d) **Mradi Na. 4944-** Programu ya Kuendeleza Ushindani wa Sekta Binafsi **(Fungu 37)**
e) **Mradi Na. 4494-** Programu ya Uendelezaji Mifumo ya Masoko na Huduma za Kifedha Vijijini **(Fungu 37)**
f) **Mradi Na.6207** –Programu ya Kusaidia Uchaguzi Tanzania **(Fungu 61)**
g) **Miradi Na.6218, 6581 na 4952-** Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi **(Fungu 65)**

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA OFISI YA WAZIRI MKUU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa fedha 2018/2019, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 tarehe 29 na 30 Machi, 2017. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili 2017 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi Machi 2018 katika Robo ya Tatu ya Mwaka huu wa fedha 2017/2018. Uchambuzi huu pia ulitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kiasi cha Fedha kilichopokelewa katika Miradi ya Maendeleo hadi kufikia Mwezi Machi 2018. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 ili kujua vipaumbele vya kibajeti.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati ulitazama pia eneo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa kulinganisha kiasi kilichokusanywa hadi Machi 2018 na lengo la ukusanyaji lililowekwa wakati wa kupitisha bajeti Mwezi Aprili 2017. Lengo la uchambuzi wa namna hii ni kufahamu uwezo wa Serikali katika kukusanya Maduhuli. Kamati ilitumia njia mbalimbali katika uchambuzi wake

kama kutazama hali halisi ya kila Taasisi, kujiridhisha na taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu kwenye Kamati.

### 3.2 Uchambuzi wa Taarifa Kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Bunge liliidhinisha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yenye jumla ya **Shilingi Bilioni Thelathini na Sita, Milioni Hamsini na Nne, Laki Saba Themanini na Nne Elfu (36,054,784,000/=).** Hadi kufikia Februari , 2018 kiasi cha Maduhuli kilichokusanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake ni **Shilingi Bilioni Ishirini na Moja, Milioni Mia Mbili Sitini na Moja, Sabini na Nane Elfu na Mia Mbili na Nane tu (21,261,078,208)** sawa na **asilimia 58.9** ya lengo lililokusudiwa.

### 3.3 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Mafungu yanayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake yalitengewa **Shilingi Bilioni Sitini na Saba, Milioni Tatu,Laki Saba na Tisa Elfu na Mia Tatu Thelathini na Sita (67,003,709,336 /=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Februari 2018 Taasisi hizo zilipokea **Shilingi Bilioni Arobaini na Tatu, Milioni Mia Tatu Arobaini na Mbili na Ishirini na Moja Elfu, Mia Tatu Tisini na Tatu (43,342, 021,393) sawa na asilimia 64.7% ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge.**

Uchambuzi wa uwiano wa Bajeti iliyoidhinishwa na upatikanaji wa fedha ya Matumizi ya Kawaida hadi kufikia Februari 28, 2018 umeainishwa katika **Jedwali Na. 1**

**JEDWALI NA. 1: Uchambuzi wa Uwiano wa Bajeti iliyoidhinishwa na Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida hadi kufikia Februari, 2018**

| NA. | FUNGU | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | FEDHA ILIYOPATIKANA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 37-OFisi ya Waziri Mkuu | 21,819,483,336 | 10,204,275,965 | 46.8 |
| 2 | 25- Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu | 5,923,228,000 | 4,228, 560,201 | 71.4 |
| 3 | 65 – Kazi, Ajira ,Vijana na Wenye Ulemavu | 11,561,196,000 | 7,239,972,429 | 62.6 |
| 4 | 27- Msajili wa Vyama vya Siasa | 19,525,938,000 | 12,768,806,400 | 65.4 |
| 5 | 15-Tume ya Usuluhishi na Uamuzi | 3,409, 750,000 | 1,991,892,331 | 58.4 |
| 6 | 61- Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 4,764,294,000 | **6,908,514,067** | **145** |
| | **JUMLA** | **67,003,889,336** | **43,342,021,393** | **64.7** |

**Chanzo: Taarifa ya WN-OWM, tarehe 27 Machi, 2018**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi huu unaonyesha kuwa kumekuwa na Mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha kwa kila Fungu. Aidha, Fedha iliyoongezeka katika Bajeti ya Fungu 61(Tume ya Taifa ya Uchaguzi) hadi kupokea

zaidi ya asilimia 100% ya fedha zilizoidhinishwa, ni kutokana na gharama za Chaguzi ndogo zilizohitaji kiasi hicho cha fedha ili kukamilisha chaguzi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Maoni ya Kamati ni kwamba hali hii ya upataikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa kuendelea na kuzingatiwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, ili kurahisisha usimaimizi na Utekelezaji wa Shughuli mbalimbali za Serikali kwa wakati na kwa ufanisi. Kwa hatua hii, Kamati inaipongeza Hazina na Serikali kwa Ujumla kwa kutoa Fedha kwa wakati kama zilivyoidhinishwa na Bunge.

## 3.4 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018,

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Ofisi ya Waziri Mkuu iliidhinishiwa Fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha **Shilingi Bilioni Tisini na Tatu, Milioni Mia Tano Sitini na Tano, Laki Tatu Sabini na Mbili Elfu , Mia Saba Sitini na Tatu(93, 565, 372, 763 )** ambapo kiasi cha **Shilingi Bilioni Sitini na Moja, Milioni Mia Tano Sitini na Tano, Laki Tatu Sabini na Mbili Elfu, Mia Saba Sitini na Tatu (61, 565, 372, 763)** ambazo ni sawa na **Asilimia 65.80%** ya Bajeti ya Maendeleo zilikuwa Fedha za Nje na **Shilingi Bilioni Thelathini na Mbili (32, 000,000,000), ambayo ni sawa na Asilimia 34.20%** ya Bajeti ya Maendeleo zilikuwa fedha za ndani.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Februari, 2018 Fedha za Miradi zilizopokelewa ni **Shilingi Bilioni Arobaini na Sita, Milioni Mia Tano Thelathini na Mbili, Laki Tano Arobaini na Tano Elfu, Mia Tisa Sabini na Tisa (46, 532, 545, 979) sawa na asilimia 49.7%** tu ya Fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Hata hivyo, kati ya fedha hizo zilizopokelewa, fedha za ndani ni **Shilingi Bilioni Nne na Milioni Shirini na Tatu Elfu, Laki Sita Ishirini na Tatu, Mia Moja( 4, 023, 623, 100)** ambazo ni sawa na **asilimia 6.54%** ya Fedha iliyokuwa imetengwa kama bajeti ya Ndani.

**Mheshimiwa Spika,** ufafanuzi zaidi kuhusu mchanganuo wa mwenendo wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ni kama inavyoainishwa katika Jedwali lifuatalo, **(Jedwali Na.2):-**

**JEDWALI NA.2: Mwenendo wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo hadi Februari, 2018**

| FUNGU | NA.YA MRADI | JINA LA MRDAI | FEDHA ZILIZOIDHINISHWA 2017/2018 | | FEDHA ZILIZOPOKELEWA HADI FEB.2018 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani | Fedha za Nje | F/Ndani | F/Nje | Asilimia % |
| 37 | 6351 | Ujenzi wa Majengo-OWM | 5,000,000,000 | 0 | 4,023,623,100 | | 80.5 |
| | 6575 | Mradi wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa | 0 | 440,000,000 | 0 | 0 | 0 |
| | 5306 | Mradi wa Kuimarisha Taarifa za Mabadiliko ya Tabianchi na Mifumo ya Tahadahari | 0 | 1,021, 618,000 | 0 | 283,986,200 | 27.80 |
| | 4944 | Programu ya Kuendeleza Ushindani wa Sekta Binafsi | 300,000,000 | 16,258,594,844 | 0 | 0 | 0 |
| | 4494 | Programu ya Uendeezaji Mifumo ya Masoko na | 700,000,000 | 42,445,159,919 | 0 | 40,957,778,948 | 95 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Huduma za Kifedha Vijijini | | | | | |
| 61 | 6207 | Programu ya Kusaidia Uchaguzi Tanzania | 10,000,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 65 | 6218 | Mradi Unaotekelezwa kwa Pamoja na ILO | 0 | 1,400,000,000 | | 319,505,139 | 23 |
| | 6581 | Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini | 15,000,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 4952 | Mfuko wa Maendeleo ya Vijana | 1,000,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA** | | | **32,000,000,000** | **61,565,372,763** | **4,023,623,100** | **42,508,922,878** | |
| | | | **93,565,372,763** | | **46,532,545,979** | | **49.7** |

**Chanzo: Taarifa ya WN-OWM, tarehe 27 Machi, 2018**

### 3.5 Yatokanayo na Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ilitegemea kwa kiasi kikubwa fedha za Nje kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 jambo ambalo likiendelea linaweza kukwamisha utekelezaji wa maendeleo ya nchi hasa ukizingatia unyeti wa Ofisi hii. Kamati inashauri Serikali kutafuta vyanzo mbadala vya ndani ya nchi katika kugharamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu badala ya kutegemea misaada kutoka nje ya nchi.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 tarehe 27 na 28 Machi 2018. ***Mpango huu wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 umeandaliwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mpango ambao umelenga utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/2021).***

### 4.1 Uchambuzi wa Vipaumbele vya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Bajeti wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 umeainisha maeneo 23 ya viapumbele yakiwemo;

i) Kuchapa Nyaraka mbalimbali za Uendeshaji wa Shughuli za Serikali Kuu, Bunge na Serikali za Mitaa,
ii) Kujenga uwezo wa Serikali kukabiliana na Maafa;
iii) Kuratibu Utekelezaji wa Mpango wa Ushiriki wa Watanzania kwenye Uwekezaji (Local Content);
iv) Kuratibu Shughuli za Bunge na kushughulikia kero na malalamiko ya Wananchi;
v) Kuboresha Mifumo ya Uchaguzi,
vi) Kumwezesha Waziri Mkuu kutekeleza Majukumu yake kwa ufaninisi Ndani na Nje ya Nchi pamoja na kuongoza Shughuli za Serikali katika Mikutano ya Bunge
vii) Kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura,
viii) Kuhakiki Maeneo ya Uchaguzi (Delimitation)

ix) Kuratibu na Kusimamia Masuala ya Fidia kwa Wafanyakazi wanaoumia, kufariki au kupata madhara ya kiafya wakiwa kazini,

x) Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini,

xi) Kuratibu Utekelezaji wa Sera, Sheria na Mikakati ya Kukuza Ajira nchini na kuongeza nafasi za Ajira za Watanzania nchi za nje,

xii) Kuratibu na kusimamia Uwezeshaji na Maendeleo ya Vijana,

xiii) Kusimamia, Kuratibu na kutoa huduma kwa Watu wenye Ulemavu, na

xiv) Kusimamia Taasisi za Umma zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliridhishwa na Vipaumbele viliyowekwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2018/2019. Aidha, Kamati imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya msingi ambayo yapo katika Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Uratibu wa Chaguzi mbalimbali nchini na kukamililisha mpango wa Serikali kuhamia Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na vipaumbele hivyo Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinaakisi Kauli Mbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwa na Tanzania yenye Viwanda ili kuweza kutengeneza Ajira kwa Wananchi wengi na kuongeza fursa mbalimbali za biashara na mapato kwa nchi na Wananchi na hivyo kupunguza utegemezi mkubwa wa kibajeti kutoka nje ya Nchi.

## 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Ofisi ya Waziri Mkuu inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni Thelathini na Tisa, Milioni Mia Nane Tisini na Saba, Mia Nane Hamsini na Tano na Mia Moja Themanini**

**na Saba (39,897,855,187/=).** ***Kiasi hicho kimeongezeka zaidi ya Bilioni 3.84 ukilinganisha na Maduhuli yaliyopangwa kukusanywa kwa mwaka wa Fedha 2017/2018. Kamati imeridhishwa na nia thabiti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu kuongeza uwezo wa ukusanyaji Maduhuli katika kuchangia pato la Taifa.***

**Mheshimiwa Spika,** Maduhuli haya yatakusanywa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu **(Fungu 37),** Tume ya Taifa ya Uchaguzi (**Fungu 61),** Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, **(Fungu 65)** na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa (**Fungu 27).** Sehemu kubwa ya Makadirio ya Maduhuli haya yatatokana na shughuli za Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali katika kuchapa Nyaraka mbalimbali za Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, pamoja na Nyaraka za matukio maalumu. Sehemu nyingine inayotegemewa kutoa Maduhuli zaidi ni Fungu 65 ambalo linahusisha Taasisi mbalimbali zilizo katika Sekta ya Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu.

**Mheshimiwa Spika**, Mchanganuo wa kiasi cha Maduhuli kinachotegemewa kukusanywa kwa kila Fungu Husika ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali lifuatalo **(Jedwalu Na.3);-**

**Jedwali Na.3; Makisio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

| FUNGU | TAASISI HUSIKA | MADUHULI YALIYOIDHINISHWA 2017/2018 | MAKADIRIO YA MADUHULI 2018/2019 |
|---|---|---|---|
| 27 | Msajili wa Vyama vya Siasa | 175,000 | 175,000 |
| 37 | Ofisi ya Waziri Mkuu | 1,010,003,000 | 1,000,000,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 61 | Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 15,000,000 | 15,000,000 |
| 65 | Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu | 35,029,605,100 | 38,882,855,187 |
| **JUMLA** | | **36,054,7883, 100** | **39,897,855,187** |

4.3 **Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba jumla ya **Shilingi Bilioni Sitini na Sita, Milioni Mia Moja Sitini na Mbili, Laki Saba Themanini na Tisa, Mia Sita Tisini na Nane (66,162,789, 698/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Kumi na Tisa, Milioni Mia Mbili, Laki Tano Sabini na Mbili Elfu, Mia Tano Tisini na Nne (19,200,572,594/=)** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi Bilioni Ishirini na Tatu, Milioni Mia Nane Ishirini na Tisa, Laki Nne Sitini na Sita Elfu na Hamsini na Moja(23,829,466,051/=)** ni Ruzuku kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Msajili wa Vyama vya Siasa na **Shilingi Bilioni Ishirini na Tatu, Milioni Mia Moja Thelathini na Mbili, Laki Saba Hamsini na Moja Elfu na Hamsini na Tatu (23, 132, 751, 053/=**) ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika mchanganuo wa Mapato na Matumizi kwa Mafungu yaliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Mafungu ambayo yametengewa fedha nyingi kuliko mengine katika Mwaka wa Fedha ujao ni Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa **(Fungu 27)** ambalo limetengewa **Shilingi Bilioni Kumi na Tisa,**

**Milioni Mia Nne na Sita,Laki Tatu Arobaini na Moja Elfu, (19,406, 341,000/=)**, Ofisi ya Waziri Mkuu **(Fungu 37)** ambalo limetengewa **Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Mia Nne Ishirini na Saba, Laki Saba Kumi na Nne Elfu (17, 427, 714,000/=)** na Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu**(Fungu 65)** ambalo limetengewa **Shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Sita Arobaini na Nne, Sitini na Saba Elfu na Mia Sita Tisini na Nane(13,644, 067,698).**

4.4 **Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake zimeombewa **Shilingi Bilioni Hamsini na Nane, Milioni Mia Saba Tisini na Moja, Laki Nne Arobaini na Moja Elfu(58,791, 441,000/=)** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizi **Shilingi Bilioni Thelathini na Moja (31,000,000,000/=)** ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni Ishirini na Saba, Milioni Mia Saba Tisini na Moja, Laki Nne Arobaini na Moja Elfu (27,791,441,000/=)** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kiasi cha Fedha za Ndani kinachoombwa kwa Miradi ya Maendeleo ni kikubwa kuliko kiasi cha Fedha za Nje ukilinganisha na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka 2017/2018 ambapo kiasi cha Fedha za Nje kilikuwa kikubwa kuliko Fedha za Ndani.

**Mheshimiwa Spika,** hatua hiyo ni ya kupongezwa kwani inaonyesha nia ya kupunguza utegemezi wa Fedha za Nje katika kufadhili Miradi ya Maendeleo ambapo wakati mwingine upatikanaji wa fedha hizo huwa siyo wa uhakika na hivyo kukwamisha utekelezaji wa Mipango ya Serikali kwa Wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, fedha iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 ni pungufu kwa zaidi ya **Bilioni 34** , pungufu ambayo ni **asilimia 37%** ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya Miradi

ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika**, Upungufu katika Bajeti ya Miradi ya Maendeleo unatokana na kukamilika kwa Ujenzi wa Makazi ya Waziri Mkuu kwa kiasi kikubwa hapa Mjini Dodoma.

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Miradi ya Maendeleo katika Mwaka huu wa Fedha umelenga katika **maeneo 7** yakiwemo:-

i) Kujenga Uwezo wa Serikali kukabiliana na Maafa
ii) Kutekeleza Mpango wa Kukuza Ujuzi na Stadi za Kazi katika Viwanda, Kilimo, biashara, Utalii, Usafirishaji, TEHAMA, Madini, Mafuta na Gesi Asilia,
iii) Kuwajengea Uwezo wa Kiuchumi Viajana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana,
iv) Kuratibu upatikanaji wa Kazi na Ajira na Staha Nchini,
v) Kuratibu Programu ya kuendeleza Mifumo ya Masoko na Huduma ya Kifedha Vijijini, na
vi) Kuendeleza Ujenzi wa Makazi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mlimwa Dodoma, na
vii) Kuimarisha Upatikanaji wa Taarifa za Mabadiliko ya Tabianchi na Mifumo ya Tahadhari.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Taarifa za Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi

zake. Aidha, Maoni na Ushauri wa Kamati umezingatia pia Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2017/2018.

5.1 **FUNGU 37-Ofisi ya Waziri Mkuu**

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa na Kamati kwa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Mwaka wa Fedha uliopita. Aidha Kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge kuhakikisha Kamati inafanya Ziara ya kikazi kukagua hatua iliyofikiwa katika Ujenzi wa Makazi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ili kujiridhisha na uthamani wa Makazi hayo na kiasi cha fedha kilichotumika.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha Miundombinu ya kazi katika Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Hata hivyo, Ofisi hiyo iendelee kuboreshwa ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kazi kwa Wafanyakazi wake na kutoa taarifa kwa Kamati kuhusu hatua za utekelekelezaji zitakazofikiwa. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa fedha zote zinazoombwa na kuidhininshwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii muhimu zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa haraka na kwa ufanisi.

iii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Zabuni za ujenzi wa Miradi ya Maendeleo zitolewe kwa uwazi (Transparent and Competitive Bidding Process) na kipaumbele kitolewe kwa Makampuni ya Ndani ya Wakandarasi yaliyokidhi vigezo na yenye uwezo wa kutekeleza na kukamilisha Miradi kwa wakati na kwa mujibu wa Mikataba ya Miradi husika.

iv) **Mheshimiwa spika**, katika Miradi yote ya Maendeleo iliyotengewa fedha Mwaka uliopita wa Bajeti (2017/2018) na ile iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha ujao (2018/2019), Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe fedha zote za Miradi ya Maendeleo zinatumika kwa tija na kwa kuzingatia Kanuni ya thamani ya fedha kwa miradi husika *(Value For Money).*

v) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuendeleza jitihada zake za kuhakikisha inapunguza kwa kiasi kikubwa utegemezi wa Fedha za Nje katika Miradi ya Maendeleo. Hatua hiyo inawezekana kama Serikali itaongeza

vyanzo vipya vya Mapato, Ujenzi na Uendelezaji wa Viwanda nchini, kuimarisha Mifumo ya Udhibiti na usimamizi wa Mapato ya Serikali na kudhibiti Matumizi ya Maliasili za nchi kwa manufaa ya Wengi.

## 5.2 Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuchukua jitihada za kutosha kusuluhisha migogoro katika Chama cha Wananchi - CUF ili kuepusha athari kubwa zinazoweza kujitokeza katika Muungano.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati pia inashauri Ofisi ya Msajili wa vyama vya Siasa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na weledi katika usimamizi na utoaji wa ruzuku kwa vyama vya siasa na kuhakikisha kwamba taratibu husika zinafuatwa katika utoaji wa ruzuku hizo.

iii) **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ifanye ufuatiliaji na ukaguzi wa Matumizi ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa ili kuhakikisha kuwa matumizi ya Ruzuku hizo yanazingatia madhumuni yaliyokusudiwa na ikibainika Ruzuku hizo zinatumika tofauti na madhumuni hayo, Chama husika kisipewe Ruzuku ili kutoa fundisho kwa vyama vyote kuzingatia matumizi stahiki ya fedha za Wananchi.

iv) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri na kusisitiza kwamba, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ihakikishe kunakuwepo na Usimamizi wa karibu kwa kufuatilia na kuchunguza mienendo inayoharibu sifa na vigezo vya Vyama vya Siasa nchini na kwamba Msajili asisite kufuta Usajili wa Chama Chochote cha Siasa kitakachokiuka Sheria, Kanuni na Taratibu za Uendeshaji wa Vyama vya Siasa hapa nchini.

## 5.3 Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)

i) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Mfuko kuhakikisha unatoa Elimu ya kutosha kwa Waajili na Wafanyakazi hususan vyama vya Wafanyakazi kwa lengo la kuhakikisha kuwa Waajili wote nchini wanazingatia matakwa

ya Sheria katika kuhakikisha Wanajiandikisha kwenye Mfuko, wanalipa Ada/Michango stahiki kwa wakati na kutoa taarifa sahihi.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Mfuko kuweka mkazo zaidi katika ulipaji fidia kwa Wafanyakazi ambalo ndilo lengo kuu la Mfuko na kuweka Mfumo mzuri wa kufanya tathmini za fidia kwa Wafanyakazi wanaopata ajali kazini na kuhakikisha kwamba malipo ya fidia yanafanyika kwa haraka kwa kila Mfanyakazi aliyetimiza vigezo vya fidia.

## 5.4 FUNGU 65 - Kazi na Ajira

i) **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kuipongeza Serikali kwa kutunga Sheria ya Kuunganisha Mifuko ya Pensheni, Kamati inaendelea kushauri kuwa, haki na maslahi ya Wanachama wa Mifuko iliyofutwa zilindwe na kutolewa kwa Wakati bila usumbufu wowote. Aidha, Serikali ihakikishe ajira za Wafanyakazi zinalindwa na taarifa za Mabadiliko ya Mifuko zitolewe haraka na kwa Wakati kwa kila Mfanyakazi na Mnufaika bila usumbufu wowote.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Mamlaka ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA) kuendelea kusimamia Afya na Usalama wa Wafanyakazi Mahali Pa Kazi na hasa kwa Wafanyakazi wanaofanya kazi katika maeneo hatarishi kama Migodini au Viwandani na kuchukua hatua kali za kisheria kwa Waajili wote wasiozingatia masuala ya Afya na Usalama wa Wafanyakazi wao.

## 5.5 FUNGU 61-Tume ya Taifa ya Uchaguzi

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuendelea kuboresha Daftari la Wapiga Kura na kuchukua jitihada za kutosha katika uboreshaji wa Daftari hili. Hatua hizi zijumuishe utoaji Elimu ya Uraia hususan uandikishaji wa Wapiga Kura kwa Vijana wengi zaidi ili waweze kutumia haki yao ya Kikatiba ya kupiga au kupigiwa kura. Hali hii itaongeza idadi ya Watanzania wengi zaidi watakaokuwa na sifa na vigezo vya kupiga kura katika chaguzi mbalimbali zinazokuja.

ii) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Tume kujitahidi kufanya kazi yake kwa Weledi ili kuendelea kuaminika kwa Wadau wake wa Uchaguzi. Hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba, inawashirikisha Wadau wa Uchaguzi wakati wa uhuishaji wa Daftari la Wapiga kura ili kuepuka migogoro isiyokuwa na tija kwa Taifa.

iii) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kwamba, Tume ihakikishe inafuatilia Wasimamizi wake wa Uchaguzi na kuwawajibisha pale wanapofanya uzembe unaosababisha madhara ambayo yangeweza kudhibitiwa mapema na msimamizi aliye makini na anayetambua na kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili vema na kwa weledi wa hali ya juu. Nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Napenda nikupongeze pia kwa umahiri wako katika kasi ya kuliendesha Bunge hili katika kutekeleza Kauli Mbiu ya **HAPA KAZI TU** na **TANZANIA YA VIWANDA** kuishauri vema Serikali kwa manufaa ya Wananchi wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Naibu Spika Mheshimiwa Tulia Ackson, Mb, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Wote kwa pamoja tunawaombea afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge Kazi, Ajira, Vijana, na Watu wenye Ulemavu, Mhe. Jenista J. Mhagama, (Mb) Naibu waziri, Mhe. Antony Mavunde, (Mb), Mhe.Stella Alex Ikupa, (Mb), Makatibu Wakuu na Wataalam wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu

kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu. **Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie Katika Hansard:-**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb – M**akamu /Mwenyekiti**
3. Mhe. George Simbachawene, Mb - Mjumbe;
4. Mhe.Joseph Kizito Mhagama, Mb-Mjumbe;
   Ally Saleh Ally, Mb - Mjumbe;
5. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe;
6. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe;
8. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe;
9. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb - Mjumbe;
10. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe;
11. Mhe. Nimrod Elirehemah Mkono, Mb - Mjumbe;
12. Mhe. Susan Peter Maselle, MB - Mjumbe;-
13. Mhe. Alfredina Apilinary Kahigi, Mb - Mjumbe;
14. Mhe. Latifah Hassan Chande,Mb - Mjumbe;
15. Mhe. Saed Ahmed Kubenea, Mb - Mjumbe;
16. Mhe. Ally Abdulla Saleh, Mb - Mjumbe;
17. Mhe. Jacqueline Kandidus Ngonyani Msongozi,Mb- Mjumbe;
18. Mhe. Bupe Nelson Mwakang’ata, Mb - Mjumbe;
19. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe;

20. Mhe. Hassan Seleman Kaunje, Mb - Mjumbe;
21. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe;
22. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb - Mjumbe;
23. Mhe. Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Emmanuel A.Mwakasaka, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Dkt.Damas Daniel Ndumbaro, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, mwisho, kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, **Ndg. Stephen Kagaigai** kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Stanslaus Kagisa, Ndg. Dunford Mpelumbe na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) Ndg. Hanifa Masaninga na Watendaji wote wa Idara hiyo kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**

4 APRILI, 2018